KIKAO CHA WAGANGA WAKUU WA MIKOA NA HALMASHAURI TANZANIA TAREHE 13-18

MAFANIKIO , CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO KATIKA MIFUMO-IDARA YA AFYA

Imeandaliwa na,

Dkt.Magreth Kagashe

DMO -Kongwa

MTIRIRIKO WA MADA

- Utangulizi
- Aina za Mifumo Idara ya Afya
- Mafanikio
- Changamoto
- Mapendekezo

UTANGULIZI

- Tanzania ni nchi inayoelekea kwenye uchumi wa kati ambao unahitaji mabadiliko makubwa ya ki elektroniki kwa kasi kubwa na.

- Idara ya Afya ni moja kati ya idara kubwa na yenye mifumo mingi ya ki elektroniki .

A. MIFUMO YA KITABIBU YA TAKWIMU

I. DHIS2- District Health Information System (DHIS2.

Huu ni mfumo unaojulikana sana na kila takwimu ya afya inaingia katika mfumo. Ni mfumo unaoisaina timu ya manejiment katika ngazi zote katika kupanga na kufanya maamuzi kulingana na Takwimu zilizoingizwa. Takwimu hizi zinaweza kuingizwa katika ngazi ya kituo au ngazi ya halmashauri

II) DVDMT – District Vaccine Data Management of Tanzania

Ni mfumo unatumika kwenye kupata taarifa za chanjo, vifaa kama friji . Mfumo unashughulika na uagizaji wa chanjo na vifaa , kujumuisha na kukusanya takwimu kutoka katika ngazi ya vituo na kuingizwa katika ngazi ya Halmasahuri na kutumwa mkoani.

III) Vaccination Information Management System- VIMS

Inashugulika na uombaji wa chanjo na vifaa kutoka Wilayani (DVs)Distric Vaccine Store , zinaingizwa kwenye mfumo, zinasambwaza kwenye vituo , inakusanya taarifa za chanjo kukuingiza kwenye mfumo katika ngazi ya Halmashauri. online

IV) TIMR -Tanzania Immunization Registry

Ni mfumo wa kurejista huduma zote za chanjo zinazotolewa kwa mtumiaji. Inamtambua mtoto kwa upekee wake, Pia inatumiaka kuagiza chanjo na vifaa vyake ktoka ngazi ya kituo kwenda katika ngazi ya wilaya /halmashauri (DVs) na kuzipokea chanjo katika ngazi ya kituo

V) eTL- Electronic Tuberculosis and Leprosy system

Ni mfumo unashugulika na uingizaji wa takwimu za kifua kikuu na ukoma tu katika ngazi ya Halmashauri. Zikishaingizwa huku zinaingizwa tena kwenye mfumo wa DHIS 2

VI) NSMIS-National Sanitation Management Information System

Ni mfumo unaoingiza takwimu za mazingira na maji hususani kwenye maswala ya kinga . Takwimu zinakusanywa kutoka kwenye jamii na institution na kuingizwa kwenye ngazi ya Halmashauri

VII) eIDSR-Electronic Integrated Disease Surveillance

Ni mfumo ulioanzishwa kwa ajili ya kutoa taarifa ya aina magonjwa yaliyopewa katika afya ya jamii na magonjwa ya milipuko. Ili kufanyia kazi na kuzuia milipuko kuenea

VIII) Sample Referral Tracking System- SRTS

Ni mfumo unaotumika maabara katika usafirishaji wa sampuli za HVL (HIV Viral Load) na ufuatiliaji wa majibu ngazi ya kituo ,

IX) Care and Treatment Clinic- CTC 2 DATA BASE

Ni mfumo unashughulikia na kuzalisha takwimu za ukimwi za mwezi na za robo ndipo ziingizwe kwenye mfumo wa DHIS 2

X) ELMIS –Electronic Logistics Management Information System.

Nimfumo mkubwa unaoshulika na uagizaji wadawa na vifaa tiba katika ngazi ya kituo na Halmashuri (R&R)

B.MIFUMO YA KIUTUMISHI NA KIUTAWALA

XI) HRHIS-Human Resource for Health Information System

Ni mfumo unaoshughulikia maswala ya kiutumishi katika kupanga , kusimamia na kuendeleza watumishi

XII) HSRS -Health Staff Recruitment System

Ni mfumo unashughulikia ajira mpya kuwaunganisha na kuwaweka katika vituo vya kazi husika

XIII) SDP-Service Delivery Point System

- Ni mfumo unaokusudia kuweka njia katika utoaji wa huduma kwenye maswala ya kiutumishi na kufanya ugatuaji wa kazi za kitumishi katika eneo la idara ya afya.
- Wakuu wa idara watatakiwa kuwapanga ajira mpya katika vituo vya kazi kwa kutumia code au namba maalumu inayotolewa na HCMIS (Human Capital Management Information System)

XIV) Work Load Indicators of Staffing Need + Prioritization and Optimization Analysisi(WISN +POA)

Huu ni mfumo unatumika kukokotoa mahitaji ya watumishi kwa kila kada katika kituo cha kutolea huduma

C: MIFUMO YA FEDHA NA MIPANGO

XV) Web Based Planrep

Ni mfumo unaoshughulika na kupanga mipango na kuweka bajeti katika ngazi zote za serikali kuanzia ngazi ya kituo na kuendelea.

XVI) Facility Financial Accounting and Reporting System(FFARS)

Ni mfumo unaotumika kudhibiti matumizi sahihi ya mapato katika kituo cha afya

Mifumo mingine ya fedha ni kama

XVII) GoTHOMIS

XVIII) EPICOR

XIX) CHF IMIS

XX) e – Claim NHIF system

MAFANIKIO

- Kufanya maamuzi sahihi zaidi katika usimamizi, uendeshaji na utoaji wa huduma katika ngazi zote za afya ya msingi
- Kudhibiti ukusanyaji na kuongeza mapato kwenye vituo
- Kuwezesha upatikanaji wa takwimu sahihi zinazofanana
- Kurahisisha wakati wa kuhakiki takwimu kulinganisha takwimu

- Upangaji sahihi wa watumishi kulingana na mahitaji na ukubwa wa kazi
- Imesaidia mipango kufanyika kwa muda mfupi na kuwa shirikishi
- Mfumo wa FFARS umewezesha matumizi sahihi kwenye vituo

- Kuwezesha kujua kama kuna magonjwa ya mlipuko na kuchukua hatua mapema
- Matumizi sahihi ya chanjo na kusaidia kutafuta watoto waliopotea mapema
- Ripoti sahihi na makisio sahihi ya dawa, vifaa –tiba, vitendanishi na vitendea kazi vya huduma

CHANGAMOTO

- Kuwepo kwa mifumo mingi isiyowasiliana DHIS 2 na GoTHomis
- Uhaba wa vitendea kazi (Computer, scanner)
- Upungufu wa watumishi bora wa TEHAMA mfumo unapogoma kupata msaada kwa haraka inakuwa ngumu
- Kutopata taarifa mapema kama kuna tatizo la mfumo kutoka vyanzo husika.

- Mifumo kufundishwa ngazi ya vituo na kufanya usimamizi kuwa mgumu.
- Baadhi ya mifumo inachagua aina ya kifaa na aina ya browser
- Maeneo mengine ya vijijini mitandao ni shida
- Imeongeza mzigo wa kazi kwa watumishi wachache waliopo.
- Kunapokuwa na mifumo mingi gharama za uendeshaji zinakuwa kubwa, fedha muda

MAPENDEKEZO

- Mifumo iweze kuunganishwa ibaki michache yenye tija.
- Mifumo iwasiliane
- Sehemu ambazo mitandao ni shida watu wa mawasiliano (simu) washirikishwe
- Wasimamizi wakuu wa Halmashauri wawe wanapata mafunzo ya kutosha ili usimamizi uimalike

- Waganga wakuu wawe na umiliki(sense of ownersship) wa hii mifumo kwamba yeye ni muhusika mkuu na anawajibika kupata takwimu sahihi na kwa wakati
- Kuwekwe utaratibu mzuri wa kupata taarifa kutoka vyanzo husika kama mfumo una hitilafu ili watu wasikeshe wanalinda mfumo

TAKWIMU SAHIHI KWA MAENDELEO YETU

- ASANTE KWA KUNISIKILIZA